

Ninafaa kutarajia nini baada ya kupata chanjo ya COVID-19?



4/2021

Huenda ukapata athari za kiasi kidogo hadi wastani, kwa siku chache. Hizi ni ishara za kawaida zinazoonyesha kwamba mwili wako unajenga kinga. Athari hizi zinapaswa kuisha baada ya siku chache. Watu wengine hawapati athari zozote ama huenda wakawa na athari baada ya dozi ya pili ambazo ni tofauti na walizopata baada ya dozi ya kwanza. Ni nadra sana kuwa na athari kali baada ya kupata chanjo.



Athari zinazopatikana sana

Mkononi katika eneo lililodungwa sindano:

- Maumivu
- Wekundu
- Uvimbe

Katika sehemu zingine zote za mwili wako:

- Uchovu
- Maumivu ya kichwa
- Maumivu ya misuli
- Kuhisi kijibaridi
- Homa au kutokwa na jasho
- Kichefuchefu au kujihisi mgonjwa tumboni

Unahitaji kupata dozi 2 za baadhi ya chanjo za COVID-19 ili kupata kinga kamili dhidi ya virusi hivyo. Ni muhimu kupata dozi zote mbili, hata kama utapata athari baada ya dozi ya kwanza. Unafaa kupata dozi zote mbili, isipokuwa kama daktari wako au anayekupa chanjo atakushauri vinginevyo.



Mwili wako huchukua muda kujenga kinga baada ya chanjo yoyote. **Inachukuliwa kwamba umepata chanjo kamili au una kinga wiki 2 baada ya kupokea dozi yako ya mwisho.** Bado unaweza kuugua COVID-19 ikiwa utaambukizwa virusi hivyo kabla ya kupata dozi ya mwisho, au ikiwa uliambukizwa kabla ya mwili wako kujenga kinga kamili. Chanjo haziathiri matokeo ya vipimo. Ili kuwalinda wengine hadi watu zaidi watakapopata chanjo, vaa barakoa ukiwa katika maeneo ya umma au ukiwa miongoni mwa watu wengi.

Vidokezo muhimu

Ni vyema zaidi kusubiri kadri ya uwezo wako kabla ya kumeza dawa zozote za kutuliza maumivu baada ya kupata chanjo. Hata hivyo, ikiwa utahitaji kumeza dawa za kutuliza maumivu au usumbufu baada ya kupata chanjo, zungumza na daktari wako kuhusu kumeza dawa zinazonunuliwa bila maagizo ya daktari, kama vile ibuprofen au acetaminophen (almaarufu Tylenol).

Ni muhimu kuendelea kumeza dawa zozote za kila siku unazotumia kwa muda mrefu, isipokuwa kama daktari wako atakwambia uache kuzitumia baada ya kupata chanjo. Huenda ikawa hatari sana ikiwa utaacha kumeza dawa unazotumia kwa kawaida.

Ili kupunguza maumivu na usumbufu katika eneo ulilodungwa:

- Wekelea kitambaa safi, chenye baridi, na unyevu kwenye eneo hilo.
- Tumia au uufanyishe mkono wako mazoezi.

Ili kupunguza athari za homa:

- Kunywa maji mengi.
- Vaa nguo nyepesi, ambazo hazitakupa joto jingi

Wakati wa kupigia daktari simu


Katika hali nyingi, ni kawaida kushuhudia athari. Mpigie simu daktari au mhudumu wako wa afya:

- Ikiwa wekundu au wororo katika eneo ulilodungwa utanza kuongezeka baada ya saa 24 (au siku 1).
- Ikiwa una wasiwasi kuhusu athari unazopata au kama hazionekani kuisha baada ya siku chache.
- Ikiwa umepokea chanjo ya Johnson & Johnson na unapata athari yoyote kati ya zifuatazo: maumivu makali ya kichwa, maumivu ya mgongo, dalili mpya za kinyurolojia, maumivu makali ya tumbo, kupungukiwa na hewa, kuvimba miguuni, kuwa na madoa madogo mekundu kwenye ngozi, au una majeraha mapya au mwepesi wa kupata majeraha.



Muulize anayekupa chanjo kuhusu jinsi ya kujisajili katika v-safe.

V-safe ni zana ya mtandaoni inayokuwezesha kufahamisha CDC ikiwa utapata athari zozote baada ya kupokea chanjo ya COVID-19. Pia unaweza kupata makumbusho ikiwa unahitaji dozi ya pili.



Tathmini ya afya ya
v-safeSM
ya baada ya chanjo



Pata maelezo zaidi kuhusu v-safe kupitia www.cdc.gov/vsafe.